

## **Fomu ya Idhini ya Hiaru: Mtoto**

Kabla ya kukusanya maudhui, tafadhali:

- **Ukurasa wa 4 na 5 ni fomu za idhini** – chapisha nakala mbili
  - nakala moja ni ya mtu anayehojiwa/kurekodiwa/kupigwa picha
  - nakala ya picha sharti ihifadhiwe pamoja na video/picha kwenye [MediaHub](#).
- **Kurasa za 1, 2 na 3 zinakupa mwongozo wa jinsi ya kueleza mchakato wa kutoa idhini**
- Tafadhali weka taarifa zinazofaa **pale ilipoelekezwa kuwekwa** na uhakikishe kuwa fomu hii imeandikwa kwa lugha inayofaa

**Fomu hii ya idhini inapaswa kuwasaidia watu kuhisi watulivu, kujenga uaminifu, kuwafahamisha kuhusu haki zao na kuboresha mtazamo wa jamii kuhusu ICRC. Idhini ya hiari inahitajika katika karibu kila hali. Tazama [mwongozo wa ICRC wa kukusanya maudhui](#) kwa uwazi**

**Unapomrekodi au kumpiga mtoto picha, ni muhimu tuzingatia kila wakati masilahi bora ya mtoto husika na kuhakikisha kuwa kukusanya kwetu maudhui hakutamdhuru kivyovyote. Hiyo ndiyo sababu majadiliano yanayoshirikisha na yanayoendelea na mtoto na mzazi/mlezi wake halali ni muhimu zaidi.**

### **Orodha Hakikishi:**

- ☐ Hakikisha kuwa mtoto na mzazi/mlezi halali wako mahali patulivu. Ikiwa mahojiano yatajumuisha taarifa nyeti, hakikisha kuwa kuna faragha ya kutosha.
- ☐ Jitambulisha wewe na mkalimani. Hakikisha kuwa mtoto na mzazi/mezi wake halali wanamwelewa mfasiri na hawana tashwishi naye akifanya ukalimani.
- ☐ Eleza sababu za wewe kuwa hapo.
- ☐ Soma maandishi ya fomu ya idhini. Sitisha palipoashiriwa ili uone ikiwa mtoto au mzazi/mlezi halali ana maswali au angependa urudie.
- ☐ Tenga muda wa kueleza zaidi taarifa muhimu ukitumia lugha inayofaa umri wa mtoto.
- ☐ Hakikisha kuwa umejumuisha wasiwasi wowote wa usalama wa muktadha mahususi ili mtoto na mzazi/mlezi halali aelewe kikamilifu hatari zilizopo kuhusiana na kusimulia hadithi yake.
- ☐ Wakumbushe kuwa wanaweza kuondoa idhini yao wakati wowote, ikijumuisha wakati wa mahojiano.
- ☐ Uliza iwapo wana maswali au wasiwasi wowote.
- ☐ Iwapo wote wanakubali<sup>1</sup>, mwombe mzazi/mlezi halali atoe idhini kwa sahihi iliyoandikwa au kurekodi video<sup>2</sup>. Hakikisha umepitia vizuizi vyovyote wanavyoweza kuomba kwenye matumizi ya picha, sauti, majina yao kamili kwenye ukurasa wa 5.
- ☐ Weka maelezo ya mawasiliano katika sehemu ya chini ya hati hii kwa ajili ya kuondoa idhini au kwa maswali/wasiwasi.
- ☐ Pakia fomu ya idhini iliyoandikwa au ya video kwenye folda pamoja na faili za mradi kwenye [MediaHub](#).

### **Mfano wa Hati:**

Ufuatao ni mfano wa hati unaoweza kutumia katika muktadha wako na malengo ya mradi wako.

---

<sup>1</sup> Ikiwa mtoto au mzazi/mlezi wake halali hajatoa idhini, hatuwezi kuwarekodi wala kuwapiga picha

<sup>2</sup> Idhini kupitia kurekodi video inaweza kutolewa ikiwa mchangiaji anapendelea

## Sisi ni nani:

Kamati ya Kimataifa ya Shirika la Msalaba Mwekundu (ICRC) ni shirika la kibinadamu linalowasaidia watu ambao wameathiriwa na mgogoro wa kivita na vurugu. Ikiwa una maswali au wasiwasi wowote kuhusu ICRC na kazi yake, tafadhali muulize mfanyakazi wa ICRC wakati wowote. Unaweza pia kupata maelezo zaidi kwenye wavuti wetu: [www.icrc.org](http://www.icrc.org)


## Ni kwa nini tunataka kumrekodi au kumpiga picha mtoto wako?

Kushiriki hali yako nasi kunaweza kuwasaidia watu wengine kuelewa vyema zaidi kinachofanyika hapa na kwenye jamii yako. ICRC inapaswa kufahamisha umma kuhusu kinachofanyika hapa. Pia tunataka kuonyesha jinsi ICRC inavyowasaidia watu ambao wameathiriwa na mgogoro na vurugu. Huenda tukatumia maudhui haya kuchanga pesa kwa ajili ya kazi yetu.

Wakati mtoto wako anasimulia hadithi yake, tunaweza kumuuliza maswali binafsi, kama vile jina lake kamili, mahali aliko, hali ya familia, na kuomba kupiga picha, video au sauti. Ni chaguo lako kila wakati kuhusu ni taarifa zipi na kiasi gani ungependa kushiriki nasi.

## Pale ambapo hadithi zao zinaweza kuonyeshwa

Ifuatayo ni mifano ya jinsi picha/video za mtoto wako zinaweza kutumiwa:





ICRC @ICRC · Oct 23  
"Now I can play with other children."

Watch how Abdulbasit's life changed after receiving his artificial legs.



1 22 63

### ☐ **Je, unafurahi ili tuendelee?**


#### **Je, ni nani anayeona au kupata data na hadithi yako?**

Umma kwa jumla, wafadhili, mashirika mengine yasiyo ya faida au mashirika ya habari. Taarifa tunayokusanya kutoka kwako zitahifadhiwa kwenye hifadhidata inayodhibitiwa na ICRC.

Baada ya kuchapisha hadithi ya mtoto wako, itapatikana ili hadhira yoyote ya umma iitazame. Hii huenda ikamaanishwa kuwa serikali, mamlaka za afya au idara ya magereza pia inaweza kuitazama. Tungependa ufanye uamuzi bora kwa ajili yako kuhusu kile ungependa kushiriki na umma.

#### **Data hii itahifadhiwa wapi na kwa muda gani?**

Huwa tunahifadhi kwa muda wote picha, video na mahojiano kwenye rekodi zetu isipokuwa utuombe tuzifute kwenye **kumbukumbu zetu za umma** kupitia barua pepe: [avarchives@icrc.org](mailto:avarchives@icrc.org) au simu: +41 22 730 33 55.



Reference : V-P-BF-E-00138

Date : 04/07/2022

Country/Region : BURKINA FASO

Caption : Province of Yatenga, town of Ouahigouya. The IC is distributing essential household goods and food aid.

Photographer : MANO, VALENTIN

Keyword : TWO-WHEELED VEHICLES; ICRC SIGN; WOM FOOD AID; CHILDREN UNDER ONE YEAR OLD; PARCEL; MATERIAL ASSISTANCE

Confidentiality level : public

Publication restrictions : publication without restriction

Copyright : ICRC

Description : More than 1,000 displaced households in Ga in the east of the country benefited from this assistance.

Resolution : 5747x3981

Orientation : Landscape



IMG\_5839.jpg

[See full details](#)

Description 1000 ménages déplacés à Gayéri assistés en biens essentiels de ménage et en vivres

Date: Imported 06/07/2022

Language Not applicable, French

Validation status Validated



☐ ***Je, mngenda nirudie chochote?***

**Maoni yako ni yapi?**

*ICRC inaruhusiwa tu kushiriki hadithi na taarifa binafsi za mtoto wako ikiwa tu umetupa idhini. Unaweza kutufahamisha taarifa ambazo umeturuhusu kushiriki. Ikiwa hadithi ina taarifa binafsi, unaweza kutufahamisha ikiwa kuna sehemu ambazo hungependa tuseme au kushiriki. Ikiwa utambulisho wa mtoto wako unahitaji kulindwa, tutafanya kila tuwezalo kulinda na kutotambulisha hadithi.*

*Hata ikiwa umetupa idhini leo, unaweza kuchagua kuondoa idhini yako wakati wowote wa mahojiano au baadaye. Ni muhimu kwako kufahamu kuwa taarifa ambayo mtoto wako anatupatia itaendelea kutumika kindani kwa ICRC hadi hadithi yake ichapishwe. Hata hivyo, baada ya kuchapishwa, taarifa binafsi zinazoshirikiwa nasi zinaweza kuzalishwa upya, kuonyeshwa na kushirikiwa na wengine. Hali hii itafanya iwe vigumu zaidi kwako kufuta data.*

**Haki zako ni zipi?**

*Ikiwa una maswali, wasiwasi au malalamiko yoyote kuhusu uchakataji wa data au taarifa binafsi, wasiliana na ujumbe wa ICRC kwa .... Ikiwa malalamiko yako hayawezi kutatuliwa, wanaweza kukuelekeza kwa Ofisi ya Ulinzi wa Data ya ICRC ([dpo@icrc.org](mailto:dpo@icrc.org)) na/au Tume ya Ulinzi wa Data ya ICRC.*

*Hasa, unaweza kuwasiliana nasi ikiwa ungependa:*

- *Kuomba kufikia data binafsi ambayo wewe na mtoto wako mmetupatia;*
- *Ikiwa ungependa kupata taarifa zaidi kuhusu jinsi ICRC huchakata data yake binafsi;*
- *Ikiwa ungependa kuondoa idhini ambayo ulitupatia;*
- *Kuomba kwamba tusahihishe au kufuta data binafsi ambayo wewe na mtoto wako mmetupatia;*

☐ ***Je, mngenda nirudie chochote?***

## Fomu ya AV ya Idhini ya Mtoto - Chapisha nakala moja ya ICRC, nyingine ya mchangiaji



ICRC

**Jumuisha:** Nembo ya ICRC kwa lugha ifaayo

**Jumuisha:** Anwani ya ujumbe

Kwa kutia sahihi kwenye fomu hii:

- Ninaelewa lengo la mchakato/ziara.
- Ninaelewa kuwa kushiriki kwa mtoto wangu kwenye mahojiano au kukataa kwake hakutakuwa na athari kwenye huduma za usaidizi/msaada tunazopokea kutoka kwa ICRC.
- Ninakubali mtoto wangu arekodiwe, apigwe picha na/au kuhojiwa bila malipo.
- Ninakubali kwamba nyenzo hii inaweza kutumiwa kwa malengo ya kutoa taarifa kuhusu masuala ya kibinadamu kote duniani katika vyombo vyote vya habari, ikiwa ni pamoja na televisheni, intaneti na filamu pamoja na malengo ya kuchangisha pesa.
- Ninakubali kwamba nyenzo hii ya mtoto wangu, jina lake, sauti na wasifu wake unaweza kutumiwa leo na siku zijazo.
- Ninafahamu kuwa wakati maudhui haya yamechapishwa, ICRC haiwezi kudhibiti jinsi yatakavyotumiwa na watu wengine.
- Ninaelewa kuwa nina haki ya kupata nakala ya picha/video na kuondoa idhini yangu wakati wowote kwa kuwasiliana na [dpo@icrc.org](mailto:dpo@icrc.org) au maelezo ya mawasiliano yaliyo hapa chini.

Vizuizi

Ninaelewa kuwa niko huru kuweka vizuizi wakati wa mahojiano haya:

- ☐ Ninatoa idhini ya kutayarishwa kwa filamu, kurekodiwa na kutumiwa kwa uso/picha ya mtoto wangu. **AU**
- ☐ Sitoi idhini ya kutayarishwa kwa filamu, kurekodiwa na kutumiwa kwa uso/picha ya mtoto wangu.
- ☐ Ninatoa idhini ya kurekodiwa na kutumiwa kwa sauti ya mtoto wangu. **AU**
- ☐ Sitoi idhini ya kutayarishwa kwa filamu, kurekodiwa na kutumiwa kwa sauti ya mtoto wangu.

Ninatia idhini ya kutumia:

- ☐ Jina la kwanza la mwanangu
- ☐ Jina la pili/familia. **AU**
- ☐ Sitoi idhini ya kutumiwa kwa jina la kwanza la mtoto wangu.

Jina la mzazi/mlezi halali .....

Sahihi .....

Mahali na tarehe .....

Jina la mfanyakazi/mpiga picha/anayerekodi video kutoka ICRC .....

Sahihi .....

Mahali na tarehe .....

*Fomu hii ya idhini au idhini iliyorekodiwa inapaswa kuhifadhiwa pamoja na mradi kwenye Media Hub*

**Maelezo ya mawasiliano na ICRC ili kuondoa idhini, kuuliza maswali au kutoa malalamiko:**  
(Unaweza kuwasiliana nasi ikiwa hutaki tena kutusimulia hadithi yako au ikiwa una maswali au malalamiko yoyote kuhusu jinsi hadithi yako inavyosimuliwa)

Anwani ya barua pepe ya mjumbe wa eneo

Anwani ya mjumbe wa eneo

Namba ya mjumbe wa eneo

Saa za kazi za mjumbe wa eneo

Jina la mfanyakazi/mpiga picha/anayerekodi video kutoka ICRC .....

Mahali na tarehe .....